

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

689

VITENDO VYA KUJIFUNZA SAYANSI

Muda: Saa 3

Ijumaa, 08 Mei 2015 asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama 40 na sehemu B na C zina alama 30 kila moja.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. **Andika Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

(Ms. namba ya mtihani)

Ukurasa wa 1 kati ya kurasa 3

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. (a) Taja magonjwa mawili ya ngozi yanayosababishwa na uchafu.
(b) Orodhesha wadudu wawili ambao mazalia yao yako kwenye uchafu wa mavazi na mwili wa binadamu.
2. (a) Taja aina mbili za vyakula hatarishi kwa meno ya binadamu.
(b) Eleza kwa kifupi hatua mbili za kusafisha meno ya binadamu.
3. (a) Fafanua neno ‘mazingira’.
(b) Taja aina mbili za mazingira ya asili.
4. Eleza njia nne za kufanya maji ya kunywa yawe safi na salama.
5. (a) Mambo gani mawili yanayoonesha ubora wa chakula?
(b) Taja makundi mawili yanayoathirika zaidi kutokana na upungufu wa virutubisho katika chakula.
6. Ainisha mambo manne yanayochangia uchafuzi wa hewa.
7. (a) Fafanua manufaa ya huduma ya kwanza kwa mtu aliyepata ajali.
(b) Njia tatu zinazosaidia kuепukana na VVU/UKIMWI ni zipi?
8. Bainisha hatua nne zinazohusika katika uandishi wa taarifa ya jaribio la kisayansi.
9. (a) Taja njia nne za kuhakikisha usalama wa watoto shulenii.
(b) Orodhesha majanga manne yanayoweza kutokea katika mazingira ya shule.
10. (a) Eleza kwa kifupi miondoko miwili ya dunia na matokeo yake kwenye mazingira.
(b) Bainisha matendo manne yanayofanywa na mwanafunzi wa shule ya elimu ya awali kila siku kabla hajaenda shule.

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka katika sehemu hii.

11. (a) Kisukari ni moja ya magonjwa yasiyoambukiza lakini ugonjwa huu umeenea sehemu nyingi duniani. Jadili chanzo na dalili za ugonjwa huo.
(b) Fafanua dalili na madhara ya ugonjwa wa pepopunda.

- (c) Tumia hoja tano kueleza umuhimu wa vipimo vya VVU/UKIMWI kwa waathirika.
12. (a) Eleza kwa kutumia mifano vitendo sita vinavyosababisha uharibifu wa mazingira.
- (b) ‘Tunza mazingira ili yakutunze’. Jadili njia sita za kutunza mazingira.
- (c) Fafanua faida tatu za uoto wa asili kwa viumbhai.
13. (a) Bainisha madhara matano ya lishe duni kwa watoto.
- (b) Fafanua njia nne za upishi wa chakula.
- (c) Eleza umuhimu wa virutubisho vinavyounda mlo kamili katika chakula.

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili** (2) kutoka katika sehemu hii.

14. (a) Eleza mambo muhimu sita ya kuzingatia unapoandaa andalio la somo.
- (b) Nini umuhimu wa azimio la kazi kwa mwalimu wa elimu ya awali?
- (c) Jadili mada ndogo tano za mada kuu ‘Usafi wa Mwili’ kama zilivyoainishwa kwenye muhtasari wa elimu ya awali wa somo la Vitendo vya Kujifunza Sayansi kwa shule za msingi.
15. (a) Kwa kutumia mifano halisi, eleza aina tatu ya zana za kujifunzia zinazosaidia wanafunzi wa elimu ya awali kujenga dhana sahihi ya walichojifunza.
- (b) Bainisha sifa za zana za kufundishia elimu ya awali.
- (c) Upungufu wa vifaa na zana za kujifunzia katika shule za msingi husababisha athari katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Jadili usemi huu ukibainisha athari zake na mbinu za kukabiliana na athari hizo.
16. (a) ‘Upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi una umuhimu mkubwa’. Thibitisha kauli hiyo ukioneshwa umuhimu wa upimaji kwa mwalimu na mwanafunzi.
- (b) Mwanafunzi wa elimu ya awali hapewi mtihani kama wale wa shule za msingi bali hupimwa maendeleo yake ya kila siku na kujazwa kwenye fomu maalum. Ukiwa mwalimu wa elimu ya awali andaa msano wa fomu utakayotumia kupima maendeleo ya mwanafunzi wako.
- (c) Eleza jinsi utakavyopima maendeleo ya mwanafunzi wa somo la Vitendo vya Kujifunza Sayansi.